JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI KIKULYUNGU
S.L.P 188,
LIWALE.
10/12/2020.

MZAZI/MLEZI WA ……

YAH: KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI KIKULYUNGU.

Hongera tunapenda kukutaarifu kuwa, umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **Kikulyungu** kwa mwaka 2021. Wewe ni miongoni mwa watoto waliopata bahati ya kuendelea na m asomo ya elimu ya sekondari hivyo unapaswa uitumie nafasi hii vyema kwa manufaa yako, familia yako na taifa kwa ujumla.

KURIPOTI SHULENI:

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** siku ya Jumatatu bila kukosa ili uwahi mafunzo ya awali ya kiingereza (Form one English orientation course) itakayotolewa kabla ya kuanza masomo ya kidato cha kwanza.

SARE ZA SHULE

WAVULANA

- Mashati mawili rangi nyeupe (mikono mifupi)
- Suruali 2 rangi ya damu ya mzee (**Upana wa suruali chini usipungue inchi 15 na isiwe ya mitindo kama vile, Modal, jeans style n.k**).Tafadhali zingatia hii ili kuepuka usumbufu.
- T-shirt 1 rangi ya damu ya mzee (zinapatikana shuleni)
- Nguo za michezo (buktana T-shirt au traki rangi ya bluu na viatu vya michezo)
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye Kamba
- Mkanda mweusi wa ngozi
- Tai rangi ya damu ya mzee

WASICHANA

- Shati mbili nyeupe mikono mifupi aina ya Tomato (**wanaovaa Hijabu, shati mbili mikono mirefu na shungi nyeupe ndefu yenye kustiri mikono na kifua mpaka magotini**)
- Sketii 2 rangi ya damu ya mzee (ndefu inayogusa vifundo/kongoo za miguu)
- T-shirt 1 rangi ya damu ya mzee (zinapatikana shuleni)
- Nguo za michezo (T-shirt au traki rangi ya bluu na viatu vya michezo)
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye Kamba na kisigino kisiwe kirefu
- Tai rangi ya damu ya mzee

MAHITAJI YA DARASANI

- Daftari 10 kubwa/counter
- Daftari moja la graph kwa ajili ya masomo ya sayansi
- Kamusi ya kiingereza kwa Kiswahili
- Kalamu ya wino nyeusi au bluu, penseli na mkebe
- Rimu ya karatasi moja kwa ajili ya mitihani ya wiki na mwezi

Chakula kwa mwanafunzi ni jukumu la mzazi au mlezi, wasiliana na ofisi ya mkuu wa shule kwa maelezo Zaidi au piga simu namba 0713966522 au 0620252482

Karibu sana.

……

SHERIA ZA SHULE

Zifuatazo ni sheria za shule

Kwenda kinyume na sheria za shule kutapelekea mwanafunzi kuadhibiwa na atimaye kufukuzwa shule. Tafadhali zisome na uzielewe vizuri sheria hizo kwa kina:

A. MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na bakaji
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji wa bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa maksudi mal iya umma
8. Kudharau bendera ya taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje yashule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga Amani na usalama wa watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi

NB: ATAKAYE HARIBU MIUNDO MBINU YA SHULE NI LAZIMA ATAGHARAMIA UKARABATI YEYE MWENYEWE NA MZAZI AU MLEZI WAKE.

B. YAFUATAYO YATEKELEZWE NA MWANAFUNZI KINYUME CHAKE NI KUADHIBIWA

1. Aheshimu wakubwa na wenzake
2. Akimbie mara tu baada ya kuitwa na mwalimu au mlezi awapo shuleni
3. Atii kengele na kufuata ratiba vizuri
4. Avae sare na mavazi mengine kwa heshima
5. Aombe ruhusa kabla ya kuondoka shuleni
6. Aonane na kuongea na wageni baada ya kupata ruhusa ya mwalimu wa zamu au mlezi husika
7. Awe mtii kwa viongozi wa serikali, shule na serikali ya wanafunzi
8. Awepo darasani wakati wote wa vipindi na ashiriki katika kazi zote za usafi au zamikono.
9. Aongee lugha ya KIINGEREZA muda wote wa masomo yake akiwa shuleni
10. Awe mlinzi na mtunzaji wa mali za umma
11. Kuheshimu na kukubali tofauti ya kidini na kiutamaduni
12. Kuwa msafi wakati wote

14. Kuwahi shuleni kwa tarehe zilizopangwa
15. Kuthamini muda

Ahsante,

IMANI MBESIGWE
MKUU WA SHULE
KIKULYUNGU SEKONDARI

MEDICAL EXAMINATION FORM
(To be completed by a medical officer)

KIKULYUNGU SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 188
LIWALE.
10/12/2020

THE MEDICAL OFFICER,
LIWALE DISTRICT HOSPITAL,
P.O BOX 28,
LIWALE.

REF…… (NAME IN FULL)

Please examine the above named personand certify his/her physical and mental fitness for being a student.

Attention should be paid on:

1. Eye sight ……
2. Hearing ……
3. Speech ……
4. Leprosy ……
5. Epilepsy ……
6. Neurosis ……
7. Pregnancy ……
8. Sexual transmitted diseases ……
9. Other serious diseases ……

Yours faithfully

……

IMANI MBESIGWE
THE HEADMASTER
KIKULYUNGU SECONDARY SCHOOL

MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by government medical officer)

I have examined the above named person and I hereby certify that findings above are correct and that the person is fit/unfit to undergo secondary studies.

……
SIGNATURE/ OFFICIAL STAMP DATE

A: TAMKO LA MWANAFUNZI KUKUBALI NAFASI

Mimi ……(jina) wa …….. (mahali)

Nakubali kujiunga kidato cha kwanza shule ya sekondari KIANGARA,Naahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule na nakubali kuadhibiwa pale itakapostahiki.

SAHIHI …… TAREHE ……..

B: TAMKO LA MZAZI AU MLEZI KUKUBALIWAJIBU WA KUSOMESHA

Mimi ……(jina) wa …….. (mahali)

Ambaye ni mzazi/ mleziwa ……(jina la mwanafunzi)

Nakubali kutimiza wajibu wangu wa kusomesha mtoto wangu kwa kumpatia mahitaji muhimu kama vile sare za shule, viatu, kalamu, madaftari,chakula pamoja na kumuhimiza kufika shuleni kama sheria za nchi zinavyoelekeza. Kazi yangu ni ……

SAHIHI …….. TAREHE ……

HATI YA KUTHIBITISHA URAIA

(Sehemu hii ijazwe katika ofisi ya mkuu wa wilaya kwa wale wanafunzi wasiokuwa na cheti cha kuzaliwa au tangazo)

Nathibitisha kwamba …….. (jina) ni raia wa ……

JINA …… SAHIHI …….

TAREHE …… MUHURI HUSIKA ……